TANGAZO LA SERIKALI NA. 33 la tarehe 20/1/2023

SHERIA YA MISITU,
(SURA YA 323)

# NOTISI

(*Imetengenezwa chini ya kifungu cha 23(1))*

NOTISI YA KUSUDIO LA KUTANGAZA MABADILIKO YA ENEO LA MSITU WA HIFADHI WA KIPEMBAWE YA MWAKA 2022

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kutangaza Mabadiliko ya Eneo la Msitu wa Hifadhi wa Kipembawe ya Mwaka 2022.

Mabadiliko ya eneo

2. Eneo la ardhi ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Gazeti la Serikali Namba 258 la mwaka 1941 linapendekezwa kubadilishwa na kusomeka na kuonekana kama lilivyoainishwa katika Ramani Na. Jb 2883 yenye Skeli 1:20000 ambayo vigingi vyake vimeainishwa katika Jedwali la Notisi hii.

Madhumuni ya mabadiliko

3. Madhumuni ya mabadiliko ni kujumuisha eneo lote la ardhi ya Hifadhi ya Msitu wa Hifadhi wa Kipembawe baada ya eneo hilo kupimwa upya kwa kutumia njia za upimaji na uchoraji ramani za kisasa kwa ajili ya uhifadhi wa baioanuwai, vyanzo vya maji na tunu za kiutamaduni ili kuendeleza madhumuni ya usimamizi, uhifadhi wa eneo la msitu na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu katika eneo la msitu.

Uhalali wa Notisi

4. Notisi hii itakuwa halali kwa muda wa siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa na ndani ya kipindi hicho mtu, kundi la watu au mwakilishi wao anaweza kwa maandishi-

(a) kupinga;
(b) kuwasilisha maoni; au

(c) kudai haki zozote zinazotokana na sheria za kimila,

kuhusiana na ardhi au mazao ya msitu au haki zozote zilizoainishwa kwenye sheria nyingine katika eneo la Msitu wa Hifadhi wa Kipembawe ambalo linapendekezwa kubadilishwa.

Uwasilishaji wa pingamizi

5. Pingamizi, maoni au madai yoyote dhidi ya tangazo la Mabadiliko ya Eneo la Msitu wa Hifadhi wa Kipembawe yawasilishwe ndani ya siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii, kwa anauani ifuatayo:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maliasili na Utalii,
S.L.P. 1351,
DODOMA.

JEDWALI


*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

MSITU WA HIFADHI WA KIPEMBAWE

*Makadirio ya eneo:* Hekta 3365.60 au Kilometa za Mraba 33.66

Unakopatikana na Mipaka

Eneo lote la hifadhi awali chini ya Eneo la Msitu wa Hifadhi wa Kipembawe linalopatikana Wilaya ya Chunya, Mkoa wa Mbeya kama lilivyochorwa katika Ramani ya Idara ya Upimaji yenye Skeli 1:20000 iliyohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Upimaji na Ramani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dar es Salaam na lenye mipaka ifuatayo:




Dodoma
12 Desemba, 2022

PINDI H. CHANA,
*Waziri wa Maliasili na Utalii*